

# Wewe Ni Mnyoofu Kadiri Gani?

Fikiria matokeo ya kuwa mnyoofu na kutokuwa mnyoofu.



## UTAFANYA NINI?

**Utafanya kama ulivyoambiwa na kaka yako.** Wazazi wakikuuliza, utawadanganya ili kumlinda kaka yako.

**Mwambie kaka yako kwamba hutadanganya.** Akiamua kuondoka, waambie wazazi wako.

Matokeo mabaya ikiwa wazazi wako watagundua kwamba uliwadanganya:

---



---



---

Faida ambayo huenda ukapata ikiwa utawaambia ukweli wazazi wako:

---



---



---

“Wazazi wako watakuamini zaidi ikiwa una kawaida ya kusema ukweli.”



—Natasha.

(Soma Zaburi 119:163. Fikiria jinsi unavyohisi kuhusu kusema uwongo wa aina yoyote.)

# 2

Nimetenda dhambi.  
Dhamiri yangu inaniuma!

## UTAFANYA NINI?

**Sitamwambia** yeyote.

**Nitamweleza** mzazi au Mkristo mkomavu.

Madhara ambayo huenda ukapata  
usipomwambia yeyote:

---

---

---

Faida ambayo huenda ukapata  
ukimweleza mtu:

---

---

---

“Ukificha kosa lako, hautakuwa na dhamiri safi, na hiyo ni hisia mbaya sana. Kwa kuongezea, ukweli utakapojulikana—sikuzote ukweli haufichwi—mambo yatakuwa mabaya zaidi.”



—Carly.

(Soma Mhubiri 12:14 na Yakobo 5:14-16. Fikiria jinsi utakavyohisi vizuri baada ya kupokea msaada unaohitaji.)

3

Wewe!  
Nipe jibu la swali  
hili la mtihani!



### UTAFANYA NINI?

**Utampa;** kwa sababu hutaki kuonekana kuwa mwadilifu.

**Unakataa kuiba mtihani,** bila kujali maoni ya wanafunzi wenzako.

Madhara ambayo huenda ukapata ukimsaidia mwanafunzi mwenzako kuiba mtihani:

---

---

---

Faida ambayo huenda ukapata kwa kukataa kumsaidia mwanafunzi mwenzako kuiba mtihani:

---

---

---

“Kutokuwa mnyoofu ni sawa na kutumia dawa ya kulevya. Ukizoea kutokuwa mnyoofu, inakuwa tabia yako. Kisha unakuwa utu wako.”



—Karen.

(Soma Methali 29:25. Fikiria jinsi utakavyohisi vizuri baada ya kujitahidi kuwa mnyoofu.)

Sasa, fikiria hali inayoweza kukushawishi kutokuwa mnyoofu. Andika faida na hasara utakazopata kutokana na matendo yako.

## HALI:

### UNGEWEZA KUFANYA HIVI:

### UNGEPASWA KUFANYA HIVI:

## MATOKEO

Mabaya:

Mazuri:

Jambo kuu: Kiwango cha unyoofu ulicho nacho kinaonyesha utu wako uliyo. Hivyo jiulize hivi: 'Ninataka nijulikane kama nani kwa wengine? Kwa kweli, ninataka kuwa mtu wa aina gani?'—Methali 20:11.